

LAIKIPIA



UNIVERSITY

UNIVERSITY EXAMINATIONS

1ST SEMESTER 2025/2026 ACADEMIC YEAR

FIRST YEAR EXAMINATIONS FOR THE DEGREE OF BACHELOR OF ARTS KISWAHILI AND COMMUNICATION (KICO GROUP)

KISW 112: HISTORIA NA MAENDELEO YA KISWAHILI

STREAM: R

TIME: 2 HRS

DAY: FRIDAY (11.30AM-1.30PM)

DATE: 30/01/2026

THIS QUESTION PAPER CONSISTS OF THREE (2 PAGES)

PLEASE DO NOT OPEN UNTIL THE INVIGILATOR SAYS SO.

MAAGIZO:**JIBU MASWALI MATATU PEKEE, SWALI LA KWANZA NI LA LAZIMA****SWALI LA KWANZA (LAZIMA)**

1. (a) Thibitisha kuwa Kiswahili ni lugha ya Kiafrika yenye asili ya Kibantu kwa kutoa mifano mwafaka. **(alama 20)**
- (b) Fafanua kwa kikamilifu fasili mbalimbali zinazoeleza kuhusu asili ya Waswahili na lugha yao ya Kiswahili. **(alama 10)**

SWALI LA PILI

2. (a) Sera ya lugha ya Waingereza ilitinga ukuaji na ueneaji wa lugha ya Kiswahili nchini Kenya. Jadili kauli hii kwa tafsihi. **(alama 10)**
- (b) Fafanua sababu zilizotatiza kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Uganda kabla ya uhuru. **(alama 10)**

SWALI LA TATU

3. (a) Huku ukitoa mifano toshelevu, fafanua mbinu mbalimbali zinazotumiwa kuundia msamiati na istilahi za Kiswahili. **(alama 10)**
- (b) Jadili changamoto mbalimbali zinazokumba watafiti wanapojaribu kuhesabu na kuainisha lahaja za Kiswahili. **(alama 10)**

SWALI LA NNE

4. (a) Eleza maana ya “usanifishaji wa lugha.” **(alama 2)**
- (b) Ni hatua gani muhimu hufuatwa wakati lugha inaposanifishwa? **(alama 8)**
- (c) Hapana budi kusanifisha Kiswahili upya. Tetea kauli hii. **(alama 10)**

SWALI LA TANO

5. *“Wacha nikushow msee, maze mambo yamekuwa noma sana siku hizi. Gava ni kama imetupiga chenga sisi maGen-Z. Yaani unakaa mwezi mzima bila kupata wira au hata kugusa kachwani joo! Hata kufeast kwenyewe ni ngori bin buta men. Huu ufala utaisha siku jamo.*

- (a) Fafanua maana ya lugha iliyotumika kwenye makala haya. **(alama 2)**
- (b) Kwa kutumia mifano mitatu iliyoelezwa vyema, toa sababu zilizochangia kuzuka kwa lugha uliyoitaja katika sehemu ya (a). **(alama 6)**
- (c) Eleza namna lugha uliyoitaja hapo juu hutatiza maendeleo ya Kiswahili nchini Kenya na hatua zinazoweka kuchukuliwa ili kuikabili. **(alama 12)**